

KAZI YA LIKIZO KIDATO CHA NNE

Maagizo-

- Jibu maswali yote.
- Majibu yote yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.
- Kila swali ni alama ishirini.

SEHEMU YA A : FASIHI SIMULIZI

- 1.
- | | |
|--|------------|
| a) Fafanua maana ya lakabu | (alama 2) |
| b) Sifa za lakabu ni zipi | (alama 5) |
| c) Kwa nini lakabu ni muhimu katika jamii? | (alama 3) |
| d) Jadili manufaa ya utafiti katika fasihi simulizi. | (alama 10) |

SEHEMU B: HADITHI FUPI

Mapambazuko ya Machweo na Hadithi nyingine

2. Eleza nafasi ya vijana na wazee katika hadithi ya Mapambazuko ya machweo. (alama 20)
Nafasi ya vijana
3. ‘Sasa ni saa ngapi? Si wajua mtoto angali anakusubiri? Mtoto analala!’
- | | |
|--|------------|
| a) Eleza muktadha wa dondo hili | (alama 4) |
| b) Bainisha mtindo katika dondo hili | (alama 3) |
| c) Eleza umuhimu wa msemaji katika kuendeleza maudhui katika hadithi ya Harubu ya maisha. | (alama 10) |
| d) Kwa hoja tatu, eleza umuhimu wa msimulizi katika kuendeleza hadithi ya mzimu wa kipwerere | (alama 3) |

SEHEMU C: BEMBEA YA MAISHA NA TIMOTHY AREGE

4. “...haikuwa mara moja mnavyofikiria. Ilianza pale chuoni. Wenzangu walinipa mvinyo kunirai kuonja ulevi.”
- | | |
|--|------------|
| a) Eleza maudhui manne yanayo jidokeza katika dondo hili. | (alama 4) |
| b) Eleza athari za mhusika anayerejelewa kujitosa katika suala linalooredheshwa kwenye dondo. | (alama 6) |
| c) Kwa kurejelewa mifano tano katika tamthilia ya Bembea ya maisha, eleza tofauti iliopo katika maisha ya ndoa ya zamani na sasa | (alama 10) |
5. Jadili sababu kumi zilizompeleka mwandishi T. Arege kuandika Tamthilia hii. (alama 20)

SEHEMU D : NGUU ZA JADI NA PROFESA CLARA MOMANYI

6. “Samahani... Nina shida kidogo. Ninaomba usaidizi. Sikuwa nikilipa ushuru katika biashara zangu. Sasa wanataka kuzifunga na kunipeleka kotini.”
- | | |
|--|------------|
| a) Eleza muktadha wa dondo | (alama 4) |
| b) Bainisha toni katika dondo hili | (alama 2) |
| c) Msemaji wa maneno haya na wengine ni adui ya wananchi wa Matuo. Eleza ukweli wa kauli hili. | (alama 14) |

7. Matumizi mabaya ya mamlaka ni tatizo sugu sana katika mataifa mengi ya Afrika yanayoendelea kiuchumi. Kwa kutolea hoja mwafaka, tetea ukweli wa kauli kwa mujibu wa riwaya ya nguu za jadi. (alama 20)

8. **SEHEMU E: USHAIRI**

Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.

Jiulize ni kwa nini, uanzapo kuongea
 Sana sana makundini, watu hukuondokea
 Ndugu ujitathmini, hakika umepotea
 Sisi twakuombea, mwenye damu ya kunguni!

Mwenye damu ya kunguni, nayo lugha ya ajuza
 Wengi hawamtamani, maneno yake yaliza
 Yeye ana walakini, dosari kuliko pweza
 Kama wewe umefunza, sote hutuona duni!

Sote hutuona duni, na hilo tumezowea
 Kazi zetu zote guni, yeye tu amebobea
 Umewachokoza mbuni, mateke anapokea
 Sisi twakuombea, upae hadi hewani!

Upae hadi hewani, ujione kama bingwa
 Mewashinda gazetini, wandishi kwako wapingwa
 Yeye kwetu mpinzani, metia mipaka tingwa
 Twakuombea mtafiti, hesabu hadi mizani!

Hesabu hadi mizani, utunge kwa kukosoa
 U hodari hesabuni, nasi tushakuzoea
 We nduli kwa majirani, na waja mekutegea
 Kurekebisha hujui, ywatanika peupeni!

Ywatanika peupeni, ywajisifu mijauji
 Amezidi zetu mboni, na amevijunjia mji
 Twamwachia waamuzi, kesi wasome majaji
 Sisi twakuombea, sirekebike kidogo!

- a) Eleza ujumbe unaojitokeza katika shairi hili (alama 6)
- b) Tambua miundo wa shairi hili (alama 4)
- c) Tambua bahari ya shairi hili kwa kuzingatia mpangilio wa maneno. (alama 2)
- d) Andika ubeti wa tatu kwa lugha nathani (alama 4)
- e) Tambua aina tatu za takriri zinazojitokeza (alama 3)
- f) Onyesha toni ya shairi hili (alama 1)